

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Wizara ya Afya

Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma

**REJESTA YA UFUATILIAJI WA WAGONJWA WA
TB NA UKOMA WALIOKATIZA/ HAWAKUANZA
MATIBABU**

Jina la Kituo: _____ Halmashauri: _____ Mkoa: _____

Rejesta ya ufuatiliaji wa wagonjwa wa TB na Ukoma waliokatisha/wasioanza matibabu: TB/LEP 13 B

Rejesta hii inatumika kusajili wagonjwa wa TB au ukoma waliokatisha/wasioanza matibabu. Wagonjwa wote waliokatisha matibabu ya Kifua Kikuu au Ukoma katika kituo cha kutolea huduma za afya na wale ambao hawakuanza matibabu wanatakiwa kuorodheshwa kwenye rejesta hii. Rejesta hii pia inatunza taarifa za matokeo ya ufuatiliaji na hatua zilizochukuliwa. Rejesta hii inajazwa na watoa huduma za afya katika jamii (vikundi vya watu waliougua kifua kikuu na kupona, watoa huduma ngazi ya jamii na asasi za kiraia). Rejesta hii hutunzwa katika kituo cha kutolea huduma za afya.

Hakikisha sehemu zote zinajazwa ipasavyo.

NAMNA YA UJAZAJI

Jina la kituo: Andika Jina la kituo ambacho rejesta hii inatunzwa, ama kituo kinachohusika na usimamizi wa kikundi hiki.

Halmashauri: Andika Jina la halmashauri taarifa zinakokusanywa

Mkoa: Andika Jina la mkoa ambako taarifa zinakokusanywa

Safu ya (1) Na.: Andika namba kwa mtiririko ukianza na namba 1 na kuendelea kila mwanzo wa mwezi.

Safu ya (2) Tarehe ya ufuatiliaji: Andika siku/mwezi/mwaka wa kusajiliwa kwa mteja katika rejesta hii

Safu ya (3) Jina la mgonjwa: Andika majina matatu (kwanza, kati na ukoo) ya mgonjwa mstari wa juu, andika namba ya usajili wa mgonjwa ya TB au Ukoma mstari wa chini.

Safu ya (4) Jinsi (Ke/Me): Andika KE kama ni mwanamke, andika ME kama ni mwanamume

Safu ya (5) Umri: Andika umri wa mgonjwa kwa miaka kamili. Iwapo mgonjwa ana umri chini ya mwaka mmoja andika sifuri (0)

Safu ya (6) Aina ya Mgonjwa anayefuatiliwa: Andika namba 1 kama ni mgonjwa wa TB na namba 2 kama ni mgonjwa wa Ukoma.

Safu ya (7) Mgonjwa anayefuatiliwa: Weka alama ya vema (√) kwenye safu pohusika, Kama hajanza matibabu ama alianza matibabu.

Safu ya (8) Mahali Mteja Anapoishi: Andika mahali mgonjwa anakotoka ama kuishi, kama ilivyoelekezwa:

Safu ya (8) i Mtaa/Kijiji: Andika Jina la mtaa/Kijiji anakoishi mgonjwa,

Safu ya (8) ii Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji/kitongoji: Andika Jina la mwenyekiti wa mtaa/Kijiji au kitongoji anakoishi mgonjwa, ama andika jina la mtu maarufu anakotoka mgonjwa.

Safu ya (8) iii Namba ya simu ya Mgonjwa na Mtu wa karibu: Andika namba ya simu ya mgonjwa na la mtu wa karibu ya mgonjwa, mfano ndugu.

Safu ya (9) Matokeo ya ufuatiliaji: Weka alama ya vema (\checkmark) katika safu husika, kama Amepatikana, Hajapatikana, Amefariki

Safu ya (10) Amerudi kwenye matibabu: Andika N kwa ndio, na H kwa hajarudi kwenye matibabu

Safu ya (11) Sababu ya kutoanza matibabu: Andika maelezo kwa ufupi, sababu ya mgonjwa kutokurudi kwenye matibabu ya kifua kikuu au Ukoma.

Safu ya (12) Jina la mtoa huduma ngazi ya jamii: Andika majina mawili ya mtoa huduma aliyemfuatilia au anayemfuatilia mgonjwa.

Safu ya (13) Maoni: Andika maoni au maelekezo mengine mfano jina la asasi na maelezo mengine muhimu.

